Mzalendo Jumatatu Novemba 16, 2025 pg 4

# LATRA yanadi wiki ya watoa huduma bora

**Na MWANDISHI WETU**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewataka wadau wa usafirishaji nchini kuendelea kujisajili kuelekea wiki ya tuzo ya watoa huduma bora itakayofanyika Novemba 24 hadi 26, mwaka huu, kwa lengo la kuchochea ushindani na utoaji huduma bora kwa wasafirishaji.

Akizungumza hayo, juzi, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo alisema tayari usajili wa washiriki umeanza kwa njia ya mtandao akiwataka wengine kuendelea kufanya hivyo.

"Maadhimisho ya wiki ya usafiri endelevu barabarani, ya mwaka huu, itafanyika viwanja vya Mnazi Mmoja kwa maonesho mbalimbali na mkutano katika Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), ambapo wanatarajia washiriki zaidi ya 800," alisema.

Alieleza kuwa, tayari kamati maalumu inaendelea kuratibu washindi wa tuzo hizo, kuhakikisha wanapatikana washindi bora kulingana na sifa.

Alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuimarisha ushindani na utoaji huduma bora na nafuu kwa wananchi kufikia malengo ya usafiri salama na endelevu duniani.

Suluo alisema uwepo wa maadhimisho hayo na wiki ya utoaji tuzo kwa wateja, imesaidia kwa sehemu kubwa katika kuimarisha usalama wa usafiri ikiwemo usafiri wa usiku ambao umeendelea kuimarika kila mwaka.

Alieleza faida za uwepo wa wiki hiyo ya tuzo kwa watoa huduma, ni wamiliki wa mabasi kuongeza ushindani kwa sehemu kubwa kwa kuleta mabasi ya kisasa kwa kuwepo mabasi ya kisasa na kuondoa migomo ya usafirishaji.

"Tuzo hizo zitalenga kuwatambua wasafirishaji, watekelezaji wa mifumo, watoa huduma za Tax mitandao, watoa huduma kupitia mfumo wa VTS na waandishi wa habari na vyombo vya habari ambazo vimefanya vizuri katika kutambua mchango wa watoa huduma," alisema.

Alisema wamefanya utaratibu wa kupata washiriki ambao wamewekwa katika makundi manane na vigezo ni ubora wa kutoa huduma, umakini wa wahudumu, uhakika wa huduma ya kampuni, usalama na ubora wa huduma kwa wateja, ubunifu na matumizi ya Teknolojia, ubora na uendelevu wa huduma, utunzaji mazingira, kutumia madereva waliokidhi vigezo.

Alieleza kila kundi wamegawanya katika makundi matatu, kwa lengo la kupata watoa huduma bora huku akitaja makundi yatakayoshiriki ni wasafirishaji wa mabasi ya mikoani, magaria ya kukodi, mabasi yaendayo mikoani na wahudumu wa mabasi, watoa huduma wa tiketi mtandao.

Kwa upande wake, Ramadhani Msangi kutoka Mabalozi wa Usalama barabarani, alisema maadhimisho hayo yamekuwa na tija kwani washiriki wamekuwa wakipata hamasa zaidi kwa kutambulika kwa utoaji huduma bora.

Rais wa Chama cha Wataalamu wa Takwimu na Usafirishaji (ALTA), Alfonce Mwingira aliishukuru mamlaka hiyo na wizara kuanzisha mchakato huo kwa huduma za usafirishaji.

CamScanner